*Kioo cha Lugha, Juz. 19(1), 2021, 109-127*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

# Jaala za Mashujaa Zinazojitokeza katika Tendi za Nanga

*Hellen Nangawe Lyamuya*[1]

## Ikisiri

Makala hii imechunguza jaala za mashujaa zinazojitokeza katika tendi za Nanga. Tendi hizo ni *Rukiza*, *Mugasha* na *Kachwenyanja*. Lengo la makala hii ni kuweka bayana jaala za hatima zilizopo katika tendi za Nanga kulingana na ontolojia ya jamii za Kiafrika. Data za makala hii zilikusanywa kutoka uwandani na maktabani. Mbinu za uchanganuzi wa matini na mahojiano zimetumika katika ukusanyaji wa data. Uchambuzi wa data umeongozwa na Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika. Matokeo ya utafiti katika tendi hizo yanaonesha kuwa mashujaa wa tendi za Nanga wanafungamana na jaala mbili za hatima. Jaala ya shujaa iliyojitokeza katika utendi wa *Rukiza* ni jaala ya ustawi wa jamii ya Baganga na jaala ya utawala. Katika utendi wa *Mugasha* kuna jaala ya bahati ya kuoa mwanamke na jaala ya utawala. Kwa upande wa utendi wa *Kachwenyanja* kuna jaala ya kutafsiri ndoto ambayo imeundwa na jaala ya bahati ya kuoa mwanamke na jaala ya kifo. Aidha, katika tendi za Nanga shujaa akifungamana vizuri na jamii yake kupitia vipengele mbalimbali vya kiontolojia anafanikiwa kutimiza jaala yake. Vilevile, shujaa akivunja mshikamano kati yake na ontolojia ya jamii yake anashindwa kutimiza jaala yake.

## 1.0 Utangulizi

Makala hii imeshughulikia nyimbo za Nanga zinazohusu mashujaa waliopo katika jamii ya Wahaya. Nyimbo hizo hujukalikana kama tendi za Nanga[2]. Ushairi huu umeitwa Nanga kutokana na ala ya muziki yenye umbo la mtumbwi na nyuzi saba ambayo inatumika wakati wa uimbaji wa nyimbo hizo. Ushairi huu wa kitamaduni unapatikana katika eneo la ukanda wa maziwa makuu kuanzia Uganda, Tanzania, Kongo na Zambia. Baadhi ya tendi za Nanga zinazopatikana katika jamii ya

[1] Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Lugha na Stadi za Mawasiliano, Kitivo cha Sanaa, Sayansi na Elimu, Chuo Kikuu cha Iringa, Tanzania. Baruapepe: Hellen_Lyamuya@yahoo.com

[2] Aidha, katika jamii ya Wahaya kuna nyimbo za Nanga zinazohusu masuala ya maadili, wanyama, ndoa na magonjwa. Nyimbo hizo si tendi kwa sababu hazijakidhi vigezo vya tendi za Kiafrika.

Tanzania ni *Rukiza*, *Mugasha*, *Kachwenyanja* na *Mugangala*. Muktadha wa kihistoria na kijamii unaonesha kuwa tendi hizo zinafungamana na utamaduni wa Wahaya (Mulokozi, 2002). Utamaduni kwa jamii za Kiafrika unafungamana na ontolojia ya Kiafrika. Kagame (1956), Mbiti (1969) na Makumba (2005) wanaeleza kuwa ontolojia hiyo inajumuisha mfumo mzima wa maisha ya watu, tamaduni pamoja na imani zinazoongoza maisha yao. Kwa msingi huo, zikiwa miongoni mwa tanzu za fasihi zinazofungamana na utamaduni wa jamii, tendi za Nanga zinajumuisha vipengele mbalimbali vya imani za jamii ikiwamo jaala. Msingi mkubwa wa ujaala ni imani ya kutoepukika kwa matukio fulani licha ya juhudi za binadamu kuyakwepa. Hii inamaanisha kuwa matukio yanayompata binadamu hutokana na mpango au utaratibu ambao binadamu hawezi kuuzuia (Wamitila, 2003). Kwa mtazamo wa ontolojia ya jamii za Kiafrika mpango huo unahusishwa na kanuni au nguvu fulani ambayo inatokana na falsafa fulani au mfumo maarufu wa imani. Nguvu hiyo huamua matukio yote au baadhi ya matukio ya maisha ya mwanadamu (Ponera, 2014; Ortega, 2016; Reehana, 2016; Charles, 2019). Hivyo, kani za kiontolojia zina mchango mkubwa katika msako wa jaala za mashujaa wa tendi za Kiafrika.

Kwa upande wa tendi za Nanga, jaala za mashujaa zinafungamana na ontolojia ya jamii ya Wahaya. Vilevile, mashujaa wamelazimika kusaka jaala zao kwa sababu kila shujaa alikuwa na malengo, matarajio na mitazamo yake juu ya maisha kulingana na ontolojia ya jamii ya Wahaya. Aidha, katika tendi nyingi za Kiafrika mashujaa wengi hupambania jaala ya hatima ya utawala. Makala hii imechunguza kwa kina jaala nyingine za hatima zinazojitokeza katika tendi za Nanga ikiwamo jaala ya utawala. Viatani vilivyotumika katika makala hii ni vile vilivyoandikwa na Mulokozi (2002). Mulokozi anaeleza kwamba kiatani cha utendi wa *Rukiza* kiliimbwa na yeli aitwaye Habibu Selemani aliyeishi miaka ya 1929-1993 na kurekodiwa na Mugyabuso Mlinzi Mulokozi mwaka 1974. Kiatani cha utendi wa *Mugasha* na utendi wa *Kachwenyanja* vyote vimeimbwa na Leonard Ngurukizi (*omutekaya*) na kurekodiwa na Paul Bateyunge mwaka 1976. Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika imetuwezesha kufafanua jaala za hatima zinazojitokeza kwenye viatani hivyo.

Ili kutimiza azma hiyo, makala hii imegawanywa katika vipengele vitano. Kipengele cha kwanza ni utangulizi. Sehemu hii inaeleza maana ya tendi za Nanga na uhusiano wa jaala za mashujaa na ontolojia ya jamii za Kiafrika. Kipengele cha pili kinahusu mbinu na nadharia iliyotumika katika utafiti. Kipengele cha tatu kinahusu uchambuzi wa data. Katika kipengele hiki tumeeleza jaala za hatima zinazojitokeza katika tendi za *Rukiza*, *Mugasha* na *Kachwenyanja*. Kipengele cha nne kinatoa mahitimisho kuhusu jaala za hatima zilizojitokeza katika tendi za Nanga. Kipengele cha mwisho kina marejeleo yaliyotumika katika makala hii.

## 2.0 Mbinu za Utafiti

Data za makala hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu za uchambuzi matini na mahojiano. Uchambuzi matini umetuwezesha kukusanya data katika matini za utendi wa *Rukiza*, *Mugasha* na *Kachwenyanja*. Matini hizo zimepatikana katika Makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa upande wa uwadani, mbinu ya mahojiano imetumika kukusanya data zilizotuwezesha kufafanua jaala za mashujaa zilizojitokeza katika tendi teule. Aidha, sampuli iliyotumika katika utafiti huu ni wapiga nanga 8, vijana 2 na wazee 10 wanaofahamu ontolojia ya Wahaya. Watoataarifa waliochunguzwa walipatikana katika mkoa wa Kagera, wilaya za Bukoba Vijijini, Muleba na Missenye. Hivyo, mbinu hizo zimetuwezesha kupata data ndani ya matini za tendi na wakazi wa mkoa wa Kagera. Data hizo zilituwezesha kueleza jaala ya shujaa inayojitokeza katika tendi za Nanga.

## 3.0 Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika

Utafiti huu umetumia Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika. Mwasisi wa nadharia hii ni Placide Tempels katika kitabu chake kinachojulikana kama *La Philosophie Bantoue* (1945). Tempels (1969) anaeleza kwamba kwa Wabantu, ontolojia ya Kiafrika inafungamana na kani uhai. Kani uhai inahusishwa na Mungu, uungu, mwanadamu na jamii. Kani hizi zinaweza kudhoofisha au kuimarisha maisha ya binadamu. Baadhi ya Waafrika walioendeleza nadharia hii ni pamoja na Kagame (1956), Mbiti (1969), Kezilahabi (1985), Makumba (2005), Mihanjo (2014) na Mulokozi (2017). Wataalamu hao wanaeleza kwamba Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika inajumuisha misingi kama vile dini, uanthropomofia, familia pana, ulimwengu wenye nyuga tatu,[3] kuheshimu wahenga au mahoka, kuthamini sana uzazi, miungu wengi, mapepo, imani katika sihiri na uchawi, uyakinifu wa kipragmantiki,[4] na dhana ya wakati. Misingi mingine ya ontolojia ya Kiafrika ni ujamiishaji wa kiduara,[5] kuthamini kazi, itikadi ya kani, mtazamo wa umosi, matambiko, nguvu hai, umoja, mshikamano na ukamilishano wa maumbile na vilivyomo na jaala badilifu. Makala hii imetumia baadhi ya misingi iliyojitokeza katika tendi teule.

Kuhusiana na msingi wa kuthamini sana uzazi, Magesa (1997) anaeleza kuwa katika jamii za Kiafrika mimba huonekana kuwa ni baraka kutoka kwa miungu au Mungu. Vilevile, uwezo wa kuzaa mtoto ni kitu muhimu katika ndoa ambayo ni

---

[3]Ulimwengu wenye nyuga tatu hujumuisha ardhi wanayoishi watu, mizimu na viumbe wengine, kuzimu wanakoishi mizimu au wahenga na juu mbinguni anakoishi Mungu na miungu (Mulokozi, 2017).

[4] Uyakinifu wa kipragmantiki ni mtazamo wa kujali zaidi hali na mahitaji ya maisha ya sasa au yajayo na kujali vitendo kuliko nadharia. Maisha ya maana ni ya duniani si yale ya baada ya kufa (Mulokozi, 2017).

[5] Ujamiishaji wa kiduara ni mzunguko wa maisha toka kuzaliwa, kuota meno, unyago, kuoa/kuolewa, uzee, kufariki, kuwa mzimu na kuzaliwa tena (Mulokozi, 2017).

kigezo cha hadhi katika jamii. Aidha, kwa upande mwingine, uzazi ni njia ya kuendeleza mduara wa maisha katika jamii za Kiafrika (Wiredu, 2006). Msingi huu umetumika kuchunguza kipengele cha uzazi kinavyohusiana na jaala za mashujaa zinazojitokeza katika tendi za Nanga.

Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika inatambua kuwapo kwa kani ambazo ni kiini cha maisha na jaala ya kila kiumbe. Kani hizo zinaweza kudhoofisha au kuimarisha maisha ya binadamu kulingana na nafasi yake. Katika ontolojia ya Kiafrika, Mungu ndiye mwenye nguvu uhai kuu na hushikilia nguvu uhai za viumbe wengine kwa viwango tofauti. Kiwango cha juu kabisa ni cha wahenga na mizimu ambao wapo karibu na Mungu. Mizimu na wahenga hutumiwa na Mungu kama matarishi na viunganishi kati ya Mungu na wanadamu. Kwa hiyo, binadamu humfikia Mungu kwa njia ya wahenga (Tempels, 1945; Mbiti, 1969; Magesa, 1997; Nkemnkia, 1999 na Mihanjo, 2004). Msingi huu unaweka bayana kuwa maisha ya mwanadamu wakiwamo mashujaa yanafungamana na kani za kijamii. Kupitia msingi huu tumebainisha vyanzo vya kani za mashujaa na nafasi yake katika msako wa jaala za mashujaa wa tendi teule.

Halikadhalika, jamii za Kiafrika huamini katika uganga na sihiri. Vipengele hivi vya kiontolojia hutumika kutatua matatizo mbalimbali yanayoikumba jamii (Ilomo, 2013; Mpalanzi, 2019). Kwa upande mwingine, uchawi ni kani ovu zenye uwezo wa kuleta madhara kwa binadamu. Katika jamii za Kiafrika uchawi huweza kusababisha magonjwa au kifo (Mair, 1969; Chuachua, 2016). Msingi huu umetuwezesha kubaini namna kani za sihiri na uganga zinavyomwezesha shujaa kutimiza jaala yake. Kwa upande mwingine, msingi huu umetumika kuchunguza jinsi kani za uchawi zinavyosababisha shujaa ashindwe kutimiza jaala yake.

Msingi mwingine uliotumika katika makala hii ni uanthropomofia. Msingi huu unahusu kumtanguliza binadamu; imani, miviga, mizimu, miungu ambayo inamhudumia mwanadamu katika mzunguko wa kuwapo hapa duniani (Mulokozi, 2017). Aidha, Mulokozi anaendelea kueleza kuwa kuheshimu wahenga hufanywa kwa njia ya matambiko ambapo wahenga hukumbukwa kwa majina katika tambizi, kutambikiwa na kuombwa msaada pale inapobidi. Mbiti (1991) anafafanua kuwa kufanya tambiko na kutoa sadaka hupatikana katika jamii nyingi za Kiafrika. Kupitia kitendo hiki, ulimwengu unaoonekana na ulimwengu usioonekana hukutana na kuakisi malengo ya mwanadamu katika ulimwengu usioonekana. Tambiko hufanywa wakati maisha ya watu yako hatarini kwa lengo la kuwaokoa na kuweka ulinzi. Msingi huu umetuwezesha kutambua njia zilizotumiwa na mashujaa wa tendi teule kutatua vikwazo wakati wa msako wa jaala zao. Vilevile, msingi huu umetupa mwanga uliotuwezesha kueleza jamii inavyowajibika kumsaidia shujaa kutimiza jaala yake.

Msingi mwingine wa Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika unasisitiza umoja, mshikamano na ukamilisho wa maumbile na vilivyomo. Wabantu wanashikilia kwamba kuna uhusiano kati ya viumbe na muumba wao. Viumbe daima hushawishiana, huvutiana na kushirikiana kwa kukusudia au kutokukusudia na

kusaidiwa na nguvu zisizo za kibinadamu au mababu. Wazo la Mwafrika la nguvu ni pamoja na mambo yote ya kimwili na kiroho. Mtu hawezi kuishi peke yake lazima awe na uhusiano na nguvu nyingine zinazomuathiri pande zote juu na chini katika mfumo wa ngazi zote za nguvu na uhai (Mihanjo, 2004). Msingi huu umekuwa faafu katika ufafanuzi wa uhusiano wa jaala za mashujaa na jamii. Fauka ya hayo, jaala badilifu ni imani katika uwezo wa mtu wa kubadilisha au kuongoza jaala au majaliwa yake (Mulokozi, 2017). Msingi huu umetusaidia kujua jaala walizopata mashujaa kutokana na jitihada zao na kuungwa mkono na jamii. Kwa ujumla, misingi tuliyoifafanua ndiyo tuliyoitumia kufafanua jaala ya shujaa inayojitokeza katika tendi za Nanga. Misingi hiyo imeteuliwa kwa sababu inafungamana na masuala ya jaala.

## 4.0 Uchanganuzi wa Data

Katika sehemu hii tunawasilisha na kuchambua data zinazohusu jaala za hatima zinazojitokeza katika utendi wa *Rukiza*, *Mugasha* na *Kachwenyaja*. Tendi hizi zimeandikwa na Mulokozi (2002) katika kitabu kiitwacho *The African Epic Controverse*. Pia, Mulokozi ametafsiri tendi hizo kutoka katika lugha ya Kihaya kwenda katika lugha ya Kiingereza.

## 4.1 Jaala Zinazojitokeza katika Tendi za Nanga

Katika tendi tulizochunguza kila shujaa alisaka jaala mbili za hatima. Katika utendi wa *Rukiza* jaala ya shujaa Rukiza ni kustawisha jamii ya Baganga na kusaka utawala wa baba yake. Kwa upande mwingine, shujaa Mugasha alisaka jaala ya mwanamke na jaala ya utawala katika utendi wa *Mugasha*. Halikadhalika, katika utendi wa *Kachwenyanja* jaala ya shujaa Kilenzi ni kutafsiri ndoto yake ambayo imefungamana na jaala ya mawanamke na jaala ya kifo. Vipengele vinavyofuata vinatoa ufafanuzi kuhusu jaala hizo kama ifuatavyo:

### 4.1.1 Jaala ya Utawala

Mashujaa wa tendi za Kiafrika huzaliwa kwa ajili ya kutimiza jaala maalumu. Baadhi ya mashujaa hutambua jaala zao na wengine hawatambui jaala zao. Katika tendi teule, shujaa Rukiza, Mugasha na Kilenzi walitambua jaala zao kwa kutumia ramli, utabiri, mizimu na masuala ya ontolojia yanayofungamana na uzazi. Kwa upande wa uzazi, Okpewho (1979) anaeleza kuwa kuzaliwa kwa shujaa kunakuwa na maajabu yanayofungamana na matukio makubwa na muhimu ambayo hayajawahi kujitokeza katika maisha ya watu wa kawaida. Matukio hayo huweka msingi wa jaala yake. Aidha, katika utendi wa *Rukiza* na *Mugasha* jaala ya utawala imedhihirika kupitia matukio ya kiontolojia yaliyojitokeza kabla ya kuzaliwa na wakati wa kuzaliwa kwa mashujaa. Shujaa Rukiza akiwa tumboni aliweza kuzungumza na kumweleza mama yake kwamba jaala yake ni kuiokomboa jamii ya Baganga na kurudisha utawala wa baba yake. Suala hili linajitokeza katika beti zifuatazo:

| | |
|---|---|
| *Ati "Oyalil'enju nk'egi*<br>*Mbwenu oshuntame onzale*<br>*Kolankeleleza ndakubalukila omulubunda!"*<br>*Ai "Nazalwa ndi Rukiza*<br>*Rukiza eilembo ly'Abaganga eli"* | Eti tandika nyumba namna hii<br>Sasa uketi unizae<br>Ukinichelewesha nitakupasukia tumboni!<br>Akasema, "ninazaliwa, ndimi Rukiza<br>Rukiza mkombozi wa kaya hii ya Baganga" |
| *Ai "Inye ndi Rukiza lwa Kilomba Kilomba kya Nyina-Mbiibi*<br>*Mbiibi eya Muzimw'Omwoija*<br>*Ndi Nkolola- Ifuta-Emilongo*<br><br>*Nazalwa ekihangula ngoma n'obwoki* | Ndimi Rukiza mtoto wa Kilomba<br>Kilomba wa Nyina -Mbiibi<br>Mbiibi wa Muzimw'Omwoija<br>Ndimi viwiko vikwanguavyo (nyuta za) *milongo*<br>Ninazaliwa mleta Ngoma na Asali |

**Chanzo:** Mulokozi (2002: 322-324)

Katika nukuu hiyo, tunaona kwamba shujaa alitambua jaala yake ya utawala kabla ya kuzaliwa. Shujaa alipata utambuzi huo kwa sababu alikuwa na nguvu za mizimu zilizomwezesha kutambua jaala yake. Vilevile, jaala ya utawala imejidhihirisha kupitia maajabu ya kitovu cha shujaa. Kitovu cha shujaa kilishindikana kukatwa kwa kutumia vifaa vya kawaida kama vitovu vya watoto wengine. Kitovu cha shujaa Rukiza kilikatwa kwa kutumia shoka. Watoataarifa walipoulizwa kuhusu shoka hilo walieleza kuwa ni shoka la kijadi. Mfano wa shoka hilo umeoneshwa katika picha namba moja.

**Picha. Na. 1: Shoka la kijadi**



**Chanzo:** Data ya Uwandani, Kijiji cha Kamachumu - Kagera, tarehe 1/5/2020

Katika ontolojia ya jamii ya Wahaya, kitovu ni sehemu yenye kani uhai na mafanikio ya mtu. Kwa hiyo, kitovu cha Rukiza kilionesha kuwa ana nguvu za sihiri na jaala

yake si ya kawaida. Pia, shujaa aliweza kukojoa mkojo uliotimua vumbi na kuwapofusha macho Wanyambo. Halikadhalika, alipojamba vumbi likawafumba macho Wanyambo. Aidha, shujaa hakunyonya kama watoto wengine bali alikunywa kianzi kizima cha maziwa ya ng'ombe. Kitendo hiki si cha kawaida kwa sababu kiasi hicho cha maziwa ni kikubwa. Mtoto mdogo hawezi kukinywa na kukimaliza chote. Picha namba mbili inaonesha kianzi cha maziwa kinachotumika katika jamii ya Wahaya.

**Picha. Na.2: Kianzi cha maziwa**



**Chanzo:** Data ya Uwandani, Kijiji cha Kamachumu- Kagera, tarehe 1/5/2020

Maajabu yaliyoambatana na kuzaliwa kwa shujaa na matukio aliyoyatenda yanadhihirisha kuwa si mtoto wa kawaida. Rukiza aliweza kufanya mambo hayo kwa sababu alikuwa na nguvu za mizimu. Nguvu hizo zilidhihirisha kuwa jaala ya shujaa Rukiza ni ya pekee. Katika utendi wa *Mugasha,* kuzaliwa kwa shujaa Mugasha kuliambatana na matukio ya kushangaza yanayofungamana na ontolojia ya jamii ya Wahaya. Shujaa Mugasha alizungumza tangu akiwa tumboni. Mugasha alimwambia mama yake atengeneze juisi ya ndizi, akate majani ya mgomba na nyasi kisha aketi amzae ili shujaa aende kuvua samaki. Nyambubi alifanya kama alivyoelekezwa na baada ya kumaliza kufanya mambo yote aliyoelezwa na Mugasha chupa ikapasuka. Suala hili limeelezwa katika beti zifuatazo:

| | |
|---|---|
| *Keyaimukile bwalukyakya si Nyambubi* | Naam, alipoamka asubuhi na mapema |
| *Aha mwalo ongw'omwabo* | Nyambubi |
| *Oguhango ogwa Nyakilembeka aaaa oooo oooo* | Pale mwaloni kwao |
| *Keyabaile naluga aha mwalo oooo* | Kwenye mwalo mkubwa uitwao |
| *Enda egya eyema omunda* | Nyalilembeke aaaa oooo oooo |
| | Alipokuwa anatoka mwaloni oooo |
| | Himila ikasema ikiwa tumboni |
| *Eti, "Mawe, eti mawe"* | Ikasema, "Mama, ikasema mama" |
| *Eti "Mawe, ahi mawe* | Ikasema, "Mama, ewe mama |

| | |
|---|---|
| *Oije ogende noiluka* | Uende ukikimbia |
| *Ogye ojunge omulamba* | Uende utengeneze togwa |
| *Ogende nailuka* | Nenda ukikimbia |
| *Ogye ojunge omulamba* | Uende utengeneze togwa |
| *Ogye ochwe enshakala* | Uende ukate majani makavu ya mgomba |
| *Oiye obunyasi onzale'nye* | Ukate na nyasi halafu unizae' mimi |
| *Nagye kujuba "nye!"* | Niende kuvua "mimi!" |
| *Yaleba yashobelwa* | Akapigwa na butwaa |

**Chanzo:** Mulokozi (2002:226-228)

Kitendo cha shujaa kuongea akiwa tumboni kinadhihirisha kuwa shujaa si mtoto wa kawaida. Pia, kuzaliwa kwa Mugasha kuliambatana na changamoto ya uzazi. Wakunga wengi hawakuweza kumzalisha Nyambubi kwa sababu viungo vya Mugasha vilikataa kutoka. Kupitia uganga walibaini mkunga atakayeweza kumzalisha shujaa. Halikadhalika, katika utendi wa *Kachwenyanja* vifaa vya kawaida kama wembe wa mianzi na kisu havikuweza kukata kitovu cha Mugasha. Uganga uliwawezesha watu kubaini kuwa kitovu cha Mugasha kitakatwa na gamba la mgomba wa *ntembe*. Vilevile, mkunga alitumia maombi kumnusuru shujaa na changamoto za uzazi. Kuhusu sababu ya kuwapo kwa maajabu ya kuzaliwa kwa mashujaa wa jamii ya Wahaya watoataarifa walidai:

> Mashujaa hawa walikuwa na nguvu za mizimu zilizotoka kwa wahenga. Nguvu za mizimu ziliwawezesha kuwa na maajabu yanayofungamana na miungu kwa upande wa uzazi. Maajabu ya kuzaliwa katika jamii yetu yalijitokeza wakati wa kuzaliwa kwa wafalme na machifu. Mtoto wa mfalme atakayezaliwa akiwa ameshika ulezi au kahawa mkononi huwa ameteuliwa na mizimu kurithi utawala wa baba yake. Mtoto huyo huchukuliwa na kufichwa ili mfalme asimuue.
>
> **Chanzo:** Mtoataarifa wa 5, mahojiano yalifanyika Muleba,
> tarehe 18/4/2020

Dondoo hili linaonesha kuwa maajabu au masuala ya kiontolojia yanayoambatana na kuzaliwa kwa watu wenye jaala ya utawala si suala geni katika jamii ya Wahaya. Katika ontolojia ya Wahaya matukio yanayoambatana na uzazi ni njia iliyotumiwa

na wakunga kubaini jaala ya utawala kwa watoto wa wafalme au machifu. Mizimu hudhihirisha jaala zao kupitia maajabu yaliyoambatana na kuzaliwa kwao. Hivyo, katika utendi wa *Rukiza* na *Mugash*a maajabu yaliyoambatana na kuzaliwa kwa mashujaa ni njia iliyotumiwa na mizimu kudhihirisha jaala yao ya utawala.

Kwa upande mwingine, jaala ya utawala ilihusisha mapambano ya vita. Mapambano hayo yaliwalazimisha mashujaa kufungamana na ontolojia ya jamii yao ili waweze kupata nguvu za sihiri. Hii ni kwa sababu mapambano ya mashujaa yalihusisha nguvu za kimwili na za kisihiri. Mulokozi (2002) anadai kuwa mapambano hayo hayawi halisi bali huwa ya kisihiri. Mapambano hayo hulenga kuonesha mtu mwenye nguvu zaidi za sihiri. Kutokana na hali hiyo, mashujaa kabla ya kwenda katika mapambano, waliomba msaada wa mizimu kwa njia mbalimbali ili kuimarisha sihiri zao. Shujaa Rukiza kabla ya kwenda vitani aliomba nguvu za sihiri kwa kumwaga mishale yake kwenye *muoto*[6] wa watoto. Suala hili limejitokeza katika ubeti wa 620.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 620 | *Rukiza tiyabandaile yajwala*<br>*Yabukwata Ekilema-Ngango*<br>*Rukiza keyashohoile Nyalulembo*<br>*Emyambi yagita aha komi y'abaana*<br><br>*Keyagizile ati "Njugunyilai nyagwe!"* | 620 | Rukiza hakukawia akavaa<br>Akakamata uta wake Kilema-Viango<br>Alipotoka nje uwandani<br>Akaweka mishale yake kwenye *muoto* wa watoto<br>Alipotamka "Nirushie nife!" |

**Chanzo:** Mulokozi (2002:256)

Katika ubeti huo *muoto* wa watoto ni chanzo cha nguvu za sihiri za Rukiza. Shujaa alimwaga mishale eneo hilo kuomba mizimu impatie nguvu za sihiri zitakazoimarisha zana zake alizozitumia katika mapambano. Nguvu nyingine za sihiri zilihifadhiwa katika kilele cha nyumba na mgomba wa *ntundu*. Shujaa Rukiza aliweza kuua watu wengi katika mapambano kutokana na nguvu zake za sihiri. Aidha, Ruhinda alitumia uchawi kubaini siri ya nguvu za sihiri za Rukiza. Ruhinda akatumia siri hiyo kutengua nguvu za sihiri za Rukiza na kusababisha shujaa Rukiza ashindwe kutimiza jaala ya utawala. Shujaa akabadili jaala yake na kujikuta anaangukia katika jaala ya kifo. Mulokozi (2002) na Lyamuya (2014) wanaeleza kuwa nguvu za sihiri ni za asili zinaweza kufanya kazi au kudhibitiwa na binadamu na mara nyingine zinaweza kushindwa na kuwa dhaifu kwa kutumia sihiri yenye nguvu sawa au zaidi. Shujaa ana uwezo wa kudhibiti nguvu zake, maarifa yake na hivyo kudhibiti jaala yake. Ili shujaa aweze kufanikiwa yeye peke yake inabidi

[6] *Muoto* wa watoto ni eneo ambalo mifugo hupumzishwa baada ya kutoka malishoni. Katika sehemu hii watu huwasha moto ambao unatumika kuchoma dawa ili moshi wake uwapate ng'ombe. Chini ya moto kuna mazindiko kwa ajili ya ulinzi wa mifugo. Sehemu hii ni miongoni mwa chanzo cha sihiri ya shujaa kwa sababu ina nguvu za mizimu na nguvu za kiganga (Mtoataarifa wa 4, mahojiano yalifanywa Muleba, tarehe 21/4/2020).

afahamu chanzo cha nguvu zake za sihiri ili aweze kubaki kama mpambanaji. Hivyo, kuna umuhimu wa kulinda chanzo cha nguvu za sihiri kwa gharama yoyote ile. Chanzo hicho kikibainika kwa adui husababisha kuanguka kwa shujaa.

Katika utendi wa *Mugasha* shujaa Mugasha kabla ya kwenda vitani aliomba mizimu ishirikiane naye katika mapambano. Shujaa Mugasha hakuwa na jeshi bali alitumia mizimu ya aina mbalimbali kupambana na adui zake. Shujaa alitumia mizimu inayofungamana na upepo, ngurumo, mvua na mwanga wa radi. Mwandishi ameonesha haya katika beti zifuatazo:

| | |
|---|---|
| *Yoooo oooo*<br>*Yayet'Embuyaga*<br>*Malonda ganobwa mushelezi atosha*<br><br>*Yayebuga nawe*<br>*"Ai "Nyenkya ninkutahila amagenyi* | Yoooo oooo<br>Akamwita Mbuyaga<br>Umande uchukiwao na mshenga asiyekinai<br>Akatamba akasema<br>"Kesho nitashiriki katika harusi yako |
| *Omwa Katanda na Katanda*<br>*Ngye ngijwengajwengye eeee*<br>*Engemu ngye nzitelanise!"*<br>*Yayeta Mushoke gwa Nyanja*<br>*Ai, "Nontahila ota amagenyi* | Nyumbani kwa Katanda na Katanda<br>Nitatikisa tikisa eeee<br>Migomba nitaikusanya pamoja!"<br>Akamwita Mushoke wa ziwani<br>Akasema, "Utashiriki vipi katika sherehe yangu |
| *Omwa Katanda na Katanda?*<br>*Ai "Ninkutahila amagenyi yo oooo*<br><br>*Kandagoba omwa Katanda na Katanda*<br><br>*Ngye ngilime empanga n'empanga'nye!*<br><br>*Ati "Naiwe nontahila amagenyi!* | Kwa Katanda na Katanda?<br>Akasema "nitashiriki katika sehemu yako yoooo<br>Nikifika nyumbani kwa Katanda na Katanda<br>Nitachimba makorongo kwa makorongo!<br>Akasema "Ukweli utashiriki katika sherehe yangu. |
| *Ayeta Nkuba Kanyalumanzi*<br>*Ati "Kyonka nontahila ota amagenyi?"*<br><br>*Ati "Inye kandagya kutaha amagenyi* | Akamwita Nkuba shujaa<br>Akasema "Utashiriki vipi katika harusi yangu?"<br>Akasema "Nitakapokwenda harusini |

| | |
|---|---|
| *Omwa Katanda na Katanda aaa* | Kwa katanda na Katanda aaaa |
| *Ngye mbabwabulikye "nye!"* | Nitawabanguabangua!" |

**Chanzo:** Mulokozi (2002:266-268)

Nukuu hiyo inaonesha kuwa Mugasha alitumia mizimu kulingana na majukumu yake. Mizimu ilimwezesha shujaa kupambana na Katanda na Katanda na kufanikiwa kutimiza jaala ya utawala. Naye shujaa Kilenzi kabla ya kwenda vitani, mke wake alimwambia ameona ishara mbaya. Shujaa alitambua kuwa hatafanikiwa katika mapambano lakini hakukubali kuacha kwenda vitani. Nyakandalo alipoona mume wake anakabiliana na jaala ya kifo, aliomba mizimu imlinde ili asidhurike akiwa vitani. Halikadhalika, shujaa Kilenzi kabla ya kwenda kwenye mapambano aliapiza kwa kutumia buni. Suala hili linadhihirika katika beti zifuatazo:

| | |
|---|---|
| *Mbona yababilikila* | Nikaona anawaapiza |
| *Waitu yanaga ensimbi n'emwani* | Akatupa simbi na buni |
| *Bojo nikwo kumala* | Akawa amemaliza |
| *Ai "Mukazi wange* | Akasema mke wangu |
| *Omuganda agila ekishoisho* | Muganda mwenye macho mazuri |
| | |
| *Omwambi Kitatela-Nte* | Mshale usiofuma ng'ombe |
| *Obutai ndataho ekyai* | Uta wangu nitaukarabati kwa kamba za migomba |
| *Zajuga zajuga omunda!* | Zimerindima zimerindima ndani! |
| Wewe | (Kazi! Kazi!) |
| | Wewe |

**Chanzo:** Mulokozi (2002:426)

Nukuu hiyo inaonesha kuwa shujaa alitumia maombi na tambiko kuomba mizimu impatie nguvu za sihiri. Shujaa alilazimika kutoa sadaka ya buni kabla ya kwenda vitani ili kuimarisha nguvu zake za sihiri. Kupitia tambiko lililoambatana na sadaka hiyo, shujaa Kilenzi aliweza kuwa na nguvu nyingi za sihiri mwilini mwake. Pia, shujaa aliweza kudaka mishale iliyorushwa na adui kwa kutumia mikono kutokana na nguvu za sihiri zilizokuwa mwilini mwake. Vilevile, katika mapambano shujaa Kilenzi aliweza kuua watu 1900 kwa kutumia mshale. Nguvu za sihiri zilimwezesha shujaa kuua adui zake Ruhinda na kulinda utawala wa Ruhinda.

Katika tendi za *Rukiza*, *Mugasha* na *Kachwenyanja* jaala ya utawala imefungamana na vipengele mbalimbali vya Ontolojia ya Kiafrika. Johnson (1992) anaeleza kuwa nguvu za siasa hazipatikani kwa nguvu za kimwili bali kwa kudhibiti nguvu za miungu. Hivyo, mashujaa walifanya jitihada za kutafuta nguvu za sihiri ili waweze kutimiza jaala ya utawala. Mashujaa waliweza kupambania jaala zao kwa sababu walikuwa wanazitambua. Utambuzi wa jaala zao ulifungamana na vipengele

vya kiontolojia na matukio ya kiontolojia yaliyoambatana na uzazi. Kwa mujibu wa Okpewho (1979), dhima ya matukio yanayotokea wakati wa kuzaliwa kwa mashujaa ni kuwatofautisha mashujaa na watu wengine. Hii ni hatua ya shujaa ambayo inaweka msingi wa jaala yake. Katika ontolojia ya jamii ya Wahaya, matukio hayo hayamaanishi kwamba jaala ya mashujaa imepangwa na mizimu bali mizimu hutumia njia hii kudhihirisha jaala ya utawala ili kuwawezesha mashujaa kutambua jaala zao. Shujaa akitambua jaala yake ya utawala huwa na uhuru wa kukubali jaala hiyo au kuikataa. Shujaa akiikubali jaala ya utawala hulazimika kupambana ili aipate. Aidha, shujaa akizembea anaweza kupoteza nafasi hiyo kama ilivyothibitika kwa shujaa Rukiza. Kwa mantiki hiyo, mashujaa katika tendi teule si wapofu wa jaala zao. Aidha, mchango wa mizimu ni kudhihirisha jaala ya utawala ila jukumu la kuipata jaala hiyo inatokana na jitihada za shujaa mwenyewe akisaidiwa na nguvu zake za sihiri.

### 4.1.2 Jaala ya Bahati ya Mwanamke

Jaala ya bahati ya mwanamke imejitokeza katika utendi wa *Mugasha* na *Kachwenyanja*. Jaala hii inahusu mapambano ya shujaa kwa lengo la kumpata mwanamke wa kumuoa. Katika msako wa jaala ya mwanamke, Mugasha alitumia vita na Kilenzi alitumia safari ya msako. Katika utendi wa *Mugasha* jaala ya shujaa Mugasha ni kumuoa dada yake Lyang'ombe ambaye hakukubali kuolewa kwa hiari na Mugasha kwa sababu alitambua kuwa Mugasha anatoka katika tabaka la chini ambalo ni la wavuvi. Mugasha akafanya jitihada za kujivua kutoka katika tabaka la chini kwa kupambana na Katanda na Katanda na kurejesha utawala wa baba yake uliokuwapo katika nchi ya Sesse. Baada ya kuchukua utawala akatumia mizimu kuendeleza mapambano na Kagoro Kemango ili kutimiza jaala ya kumuoa dada yake Lyang'ombe. Mambo haya yameelezwa katika beti zifuatazo:

*Egya emushangaho munyanya Lyang'ombe*
*Ei "Shumalamu waitu*
*Kyonka inye ekishulo tikyange*
*Neky'omwiru*
*Ow'ebitalila n'empembwe!"*

Akamkuta dada yake Lyang'ombe
Akasema "shumalamu waitu
Lakini salamu hii si ya kwangu
Nimetumwa na mtoto wa mtwana
Mwenye sharafa na nywele kifuani!"

Yamugambile
Ah "Ngu chwekamu nyabula
Ekinunki ky'olwaya
Nogya kwegomba munyanya Lyang'ombe iwe
Kwehangaza!"

Akamwambia
Akasema "Tokomea huko baradhuli
Mwenye kununka shombo
Unathubutuje kumtaka dada yake Lyang'omb
Kuvunja miiko!"

| | |
|---|---|
| *Ogitwale egi* | Ichukue nchi hii |
| *Eya Isheshe lya Katanda na Katanda!"* | Ya Sesse ya Katanda na Katanda!" |
| *Yaikiliza* | Akakubali |
| *Ai "Mubaile munjagwile* | Akasema "Mlikuwa mmenidhalilisha |
| *Kunyeta akazilo k'embungi* | Mliponiita mgaagaa |
| | |
| *Ati "Omwana wange akatwala* | Akasema "Mwanangu amechukua |
| *Engoma Omw'Isheshe!"* | ngoma huko Sesse!" |
| *Kayamanzile kutwala Engoma* | Baada ya kuchukua ngoma |
| *Ati "Kyonka ngye ngobe omwa* | Akasema "Afadhali nifike kwa |
| *Lyang'ombe* | Lyang'ombe |
| *Ngye mbonangane na munyanya* | Niende nikaonane na dada huyo |
| *Lyang'ombe ogu* | Lyang'ombe |
| *Ayanyesile ekinunki ky'olwaya "nye!"* | Aliyeniita dude lenye kunuka shombo!" |
| | |
| *Ayakwesile ekinunki ky'olwaya!"* | Aliyekuita dude linalonuka kutuzi!" |
| *Bamwiyayo* | Wakamtoa ndani |
| *Bamuhotolola bwangu* | Wakamtengeneza haraka huku |
| *Wenene ayemeleile aha butumbi* | Mugasha akiwa amesimama kilindini |
| *Lutaguza na Nshembe lwa Nyakizinga* | Mwenda Uchi na Ngawira wa Nyakizinga |

**Chanzo:** Mulokozi (2002:254, 256, 274 na 282)

Nukuu hiyo inaonesha kuwa tofauti za kitabaka ni kikwazo alichokabiliana nacho shujaa Mugasha katika msako wa jaala ya bahati ya mwanamke. Hata hivyo, shujaa alitambua kwamba njia pekee ya kuondoa tofauti hizo ni kupambana na kurejesha hadhi yake. Kupitia mapambano ya vita, shujaa alifanikiwa kurudisha utawala wa baba yake uliokuwa Sesse. Baada ya kupata utawala, shujaa alipambana na Kagoro Kemango ili kutimiza jaala ya kumuoa dada yake Lyang'ombe. Aidha, Kagoro alipambana na Mugasha kwa sababu alitambua kwamba Mugasha kumuoa dada yake anavunja mwiko. Mapambano ya Kagoro yalihusisha mishale pekee lakini mapambano ya Mugasha yalihusisha nguvu za kimwili na sihiri. Deme (2009) anadai kuwa hakuna nguvu za kibinadamu ambazo zinaweza kumshinda shujaa mwenye silaha za sihiri. Kutokana na muktadha huo, Mugasha alifanikiwa kumshinda Kagoro Kemango katika mapambano na kutimiza jaala yake ya kumuoa dada yake Lyang'ombe.

Katika utendi wa *Kachwenyanja* jaala ya shujaa Kilenzi ni kumuoa Ntuwa Nyakandalo. Jaala ya kumuoa Nyakandalo ilifungamana na ndoto. Shujaa aliota anaoa mwanamke anayeitwa Ntuwa Nyakandalo kisha akafa. Mwanamke huyo amekutana naye katika mteremko wa mlima akikata nyasi aina ya *egunga*. Shujaa akafadhaika, akamwambia mke wake ana wasiwasi kuwa hataendelea kuishi sana.

Shujaa hakufurahishwa na mambo aliyoyaota hivyo akaanza safari ya msako wa tafsiri ya ndoto yake. Tazama beti zifuatazo:

| | |
|---|---|
| *Ogu ati "Obwile tibukakeile*<br>*Mushaija wange walota otai?*<br>*Iloko ongambile okwo walota!"*<br>*Ogu ahi "Nalota ninfa*<br><br>*Waitu nalota nishwela* | Huyo mama akasema, "Bado<br>usiku Mume wangu umeota<br>nini? Kanambie uliyoota!"<br>Naye mwanamume akasema,<br>"nimeota ninakufa<br>Tena nimeota ninaoa |
| *Omukazi owo nashwela ogwo*<br>*Ni Ntuwa Nyakandalo*<br>*Namwiya omu bikiika by'eibanga*<br><br>*Nashanga nashala obunyasi*<br>*Obunyasi bwaba buli bwe'gunga* | Naye huyo mwanamke<br>niliyemuoa<br>Anaitwa Ntuwa Nyakandalo<br>Nimemkuta kwenye mteremko<br>wa mlima<br>Nimemkuta akikata nyasi<br>Nyasi za aina ya *egunga* |
| *Obunyasi bwaba buli bw'egunga."*<br>*Omukazi ogwo*<br>*Mbona yamwenya*<br>*Aiya omuganda gw'obunyasi*<br>*Waitu agwalila aha nsi* | Nyasi zilikuwa za aina ya<br>*egunga*." Huyu mwanamke<br>Nikaona anatabasamu<br>Akang'oa kitita cha nyasi<br>Bwana akakitandaza chini |
| *Baba, omukazi agya amushwela*<br>*Nyakutula, ebilo ni binai*<br>*Ekya katanu nyailya yayaluka*<br>*Keyalugile omu kisiika*<br>*Tukahulila engoma zaluta* | Baba, akamuoa yule mwanamke<br>Jamani, muishio, siku nne<br>Ya tano nyailya anatoka ndani<br>Alipotoka nje<br>Tukasikia ngoma zinarindima! |

**Chanzo:** Mulokozi (2002:396, 408 na 410)

Katika ontolojia ya jamii ya Wahaya ndoto ni njia mojawapo inayotumiwa na mizimu kuzungumza na binadamu. Kwa hiyo, mizimu ilieleza jaala ya shujaa Kilenzi kupitia ndoto aliyoota. Shujaa hakufurahishwa na ndoto hiyo, akaamua kufanya safari ya kusaka tafsiri ya ndoto yake. Katika mchakato wa kusaka jaala ya kutafsiri ndoto, shujaa alitembea umbali mrefu na mwisho alikutana na wanawake wawili chini ya mlima wakikata nyasi aina ya *egunga*. Wanawake walimuuliza anapokwenda, naye akajibu anakwenda kutafsiri ndoto yake. Baada ya kueleza ndoto yake aliyoota, Nyakandalo akakubali kuolewa na Kilenzi. Shujaa Kilenzi akafanikiwa kutimiza jaala ya kutafsiri ndoto kwa upande wa kuoa. Jaala ya kuoa iliweka msingi wa jaala ya kifo ambayo imejadiliwa katika sehemu inayofuata. Aidha, jaala ya bahati ya mwanamke katika utendi wa *Rukiza* na *Mugasha* inalenga

kuwanufaisha mashujaa wenyewe. Kwa upande mwingine jaala ya bahati ya mwanamke ilionesha kuwa mashujaa wa tendi hizi wana sifa ya urijali.

### 4.1.3 Jaala ya Kutafsiri Ndoto kuhusu Kifo

Jaala hii imejitokeza katika utendi wa *Kachwenyanja*. Shujaa Kilenzi baada ya kumuoa Nyakandalo alialikwa na Ruhinda ili akamsaidie kupambana na adui zake. Nyakandalo aliona ishara kuwa Kilenzi hatafanikiwa katika mapambano, hivyo, akamwambia ajifunge aseme ana homa ili asiende vitani. Shujaa akamwambia mke wake vita vikirindima lazima akapambane. Kwa upande mwingine, shujaa hakupenda jaala ya kifo lakini kwa sababu alikuwa na nguvu aliamua kujiingiza katika mapambano ya kusaka jaala ya hatima ya matokeo. Lightfoot (1980) anaeleza kuwa jaala ya hatima ya matokeo hujitokeza wakati shujaa anapoona dalili kuwa hatapata ushindi lakini haachi kwenda kwenye mapambano. Shujaa huweka pembeni suala la kifo na kutazama hatari ya kufa kuwa ni bora na ya thamani. Hivyo, katika utendi wa *Kachwenyanja* shujaa alikuwa katika mchakato wa kusaka jaala ya nafasi ya kufa au kuishi. Katika msako huo, shujaa alifanikiwa kuua adui wa Ruhinda na mwisho wa mapambano aliangukia katika jaala ya kukosa nafasi ya kuishi. Mwandishi ameonesha mambo haya katika beti zifuatazo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 450 | *Ebindi byaija n'omugogo*<br>*Kutema enshakala yaija n'epempe!*<br>*Ahi "Okome omutwe*<br>*Mukazi wange oyekome enkizi*<br>*Ezajuga ezizanjuga omunda* | 450 | Nyingine zimekuja na mashina<br>Nilipokata nshakala ikaja na mauzauza! Akasema, "Funga kichwa chako<br>Mke wangu kaza mwendo<br>Ngoma hizi zilizorindima zimerindima<br>Ndani mwangu |
| 455 | *Mbwenu nu*<br>*Tintwala mukama omwoi*<br>*Ntwalwa abakama bangi*<br>*Zajuga inye tindi aho*<br>*Tonmanya akabala kange* | 455 | Sasa basi<br>Sitawaliwi na mfalme mmoja<br>Ninatawaliwa na wafalme wengi<br>Zimesharindima siwezi kuwapo hapa Hunijui kijina changu |
| 685 | *Ata omu kanwa yabunyiila!*<br>*Mbwenu nu*<br>*Alugwaho akashaija* katikati<br><br>*Konene Lulyandibwa*<br>*Kashumikile olubugo lw'omushala* | 685 | Akatia kinywani na kumung'unya<br>Sasa basi<br>Kikatokea kijanaume kimoja chembamba<br>Chenyewe (kikiitwa) Lulyandibwa<br>Kimevaa lubega ya mlumba na mushala |
| | | | |

| | |
|---|---|
| *Akashaija kagalama*<br>*Kakwata obutai bwako*<br>*N'omwambi gwe'kilondano*<br>*Katela aha kanyaitolo*<br>*Omwambi gwija nigwehuba* | Kale kajanaume kakajilaza chali<br>Kakashika upinde wake<br>Na mshale wa kuokota<br>Kakapiga mshale kuelekea juu<br>Mshale ukarudi chini kasi |
| *Gwija gumukongokela*<br>*Kyakachwenyanja yakumba!*<br>*Elya kabili yakumba!*<br>*Elya kashatu yakumba!*<br>*Mbwenu baba, nyakutula* | Ukaja ukamfuma kutokea juu<br>Kachwenyanja akaanguka!<br>Mara ya pili akaanguka!<br>Mara ya tatu akaanguka!<br>Sasa baba, jamani |

**Chanzo:** Mulokozi (2002:422 na 438)

Katika dondoo hilo tunaona kuwa aliyemuua shujaa ni mtu duni, dhaifu na asiye na nguvu kama Kilenzi. Njogu na Chimerah (2008) wakijadili kuhusu majagina katika mighani mbalimbali ulimwenguni kote, wanadai kuwa licha ya maajabu na uwezo wa mashujaa, jagina huwa na unyonge mmoja kwani bado ni binadamu tu. Hufa tena kwa urahisi sana bila kuhitajika jeshi. Jagina huweza kuuawa na mtu mnyonge sana au hata mtoto mdogo. Hivyo, Lulyandibwa kumuua Kilenzi ni suala ambalo limejitokeza kwa mashujaa wengine ulimwenguni. Lulyandibwa alifanikiwa kumuua Kilenzi kwa bahati. Mizimu haikuzuia kifo cha Kilenzi kwa sababu shujaa aliomba kutimiza jaala ya kutafsiri ndoto yake kwa upande wa kifo. Katika msako wa jaala ya kutafsiri ndoto kuhusu kifo shujaa akajikuta anapoteza nafasi ya kuishi na kuangukia katika jaala ya hatima ya tanzia. Pack (1939) anaeleza kuwa katika usuli wa ontolojia ya Aristotle, jaala ya tanzia inaweza kuwasilishwa katika mpangilio wa matendo yanayoleta madhara na kuyaweka kama jaala ya kukosa nafasi au bahati. Kutokana na maelezo ya Pack katika msako wa nafasi ya kuishi au kufa shujaa Kilenzi aliangukia katika hatima ya kukosa nafasi ya kuishi. Aidha, hatima ya kukosa nafasi ya kuishi ilizua hatima ya tanzia. Kwa upande mwingine, hatima ya kifo imemwezesha shujaa Kilenzi kutimiza jaala ya kutafsiri ndoto yake kwa upande wa kifo.

### 4.1.4 Jaala ya Bahati ya Ustawi

Jaala ya ustawi ni miongoni mwa jaala iliyojitokeza katika utendi wa *Rukiza*. Airoboman (2002) anaeleza kuwa jaala ya bahati ya mtu inaweza kubadilika au kutobadilika na inaweza kuwa majumui au binafsi. Katika utendi wa *Rukiza* jaala ya ustawi wa jamii ya Baganga ni jaala ya kijamii. Rukiza baada ya kuzaliwa hakuridhishwa na hali ya maisha ya jamii yake. Jamii ya Baganga ilikuwa na ufukara uliosababisha watu kukosa chakula. Shujaa Rukiza akaamua kusaka jaala ya kustawisha jamii ya Baganga kwa sababu aliamini kuwa anaweza kuleta mabadiliko katika jamii yake. Omokpo na Ukwamedua (2016) wanadai kuwa kuna hatima

ambayo inabadilika. Hatima hiyo inatokana na matakwa ya mtu, nguvu na ushirikiano wa mtu na miungu unaomwezesha kufanikiwa na kustawi katika maisha. Hivyo, katika msako wa jaala ya kustawisha jamii ya Baganga, Rukiza na jamii yake walishirikiana katika shughuli za ufugaji na kilimo. Suala hili halijaelezwa wazi katika utendi wa *Rukiza* ila tumelibaini kutokana na maelezo yanayodai kwamba shujaa alikuwa na ng'ombe pia aliweza kukarabati upinde wake kwa kamba ya mgomba. Kutokana na kuwapo kwa vitu hivyo, ni wazi kuwa jamii ya Baganga ilijihusisha na kilimo na ufugaji. Aidha, katika msako wa jaala ya kuboresha maisha ya Baganga, shujaa alitoa tambiko la mtwana kwa kumpiga mshale mtwana na kumuua. Katika mahojiano watoataarifa walieleza:

> Tambiko la mtu lilihusisha watwana ambao ni watu wa tabaka la chini. Katika jamii yetu watu walikuwa wanatolewa kama sadaka. Mukama aliagiza mtu huyo atolewe sadaka mfano kwenye ziwa au porini kwenye tingatinga. Watu walikuwa wanauliwa ili watu wengine wapone. Matambiko yalikuwa ni sehemu ya dini za jadi. Katika jamii ya Wahaya tambiko la mtoto wa kiume lilitolewa katika uanzishaji wa ikulu ya ufalme. Mtoto mdogo wa kiume alifukiwa katikati ya nyumba ya mfalme akiwa hai na akiwa amekaa kwenye kiti. Tambiko hili lilitokana na maelekezo ya mizimu na lengo lake ni kulinda ikulu ya mfalme.

**Chanzo:** Mtoataarifa wa 7, mahojiano yalifanyika Missenye, tarehe 10/4/2020

Taarifa hiyo inaonesha kuwa matambiko ya watu yalikuwa na dhima maalumu katika ontolojia ya jamii ya Wahaya. Aidha, tambiko alilotoa Rukiza lina uhusiano na tambiko lililokuwa linafanywa na wafalme. Katika utendi wa *Rukiza* tambiko la mtwana lilitolewa na Rukiza kwa lengo la kuanzisha kaya mpya katika eneo la Byantanzi na kustawisha jamii yake. Kutokana na sadaka ya mtwana, jamii ya Baganga ilipata ulinzi dhidi ya kani ovu katika mifugo na mazao yao, jambo ambalo limewawezesha kuondoa ufukara katika jamii yao. Aidha, Rukiza alitoa tambiko kwa sababu alitambua kuwa nguvu za kimwili pekee haziwezi kustawisha jamii ya Baganga. Ushirikiano mzuri kati ya shujaa, watu na mizimu ulimwezesha Rukiza kubadili jaala ya jamii yake kwa kuitoa katika ufukara na kuistawisha. Baganga wakamjengea Rukiza ufalme kama zilivyo falme nyingine. Shujaa Rukiza akafanikiwa kutimiza jaala ya bahati ya ustawi wa jamii ya Baganga.

## 5.0 Hitimisho

Katika tendi za *Rukiza*, *Mugasha* na *Kachwenyanja*, tumebaini kuwa kila shujaa ana jaala mbili za hatima. Baadhi ya jaala zinafanana kati ya shujaa mmoja na mwingine na jaala nyingine hazifanani. Jaala tulizozibaini katika utendi wa *Rukiza* ni jaala ya utawala, bahati ya ustawi wa jamii ya Baganga na kifo. Katika utendi wa *Mugasha* kuna jaala ya utawala na bahati ya mwanamke. Kwa upande wa utendi wa

*Kachwenyanja,* kuna jaala ya kutafsiri ndoto kuhusu bahati ya mwanamke na kifo. Mashujaa wote wamefungamana na vipengele mbalimbali vya ontolojia ya Kiafrika katika msako wa jaala zao. Suala hili linadhihirisha kuwa jaala hizi zimefungamana na ontolojia ya jamii ya Wahaya na hazina athari yoyote ya ontolojia ya jamii za kigeni. Kwa ujumla, jaala ya mashujaa katika tendi hizi imefungamana na masuala ya kijadi yaliyopo katika jamii ya Wahaya na jamii nyingine za Kiafrika.

**Marejeleo**

Airoboman, F.A. (2002). The Concept of Destiny and its Social Implications among the Esans. Katika *Jorind*, Juz. 10, 3: 218-226.

Charles, A. (2019). Mvutano kati ya Maarifa ya Kijaala na Maarifa ya Kijarabati katika Maudhui ya Filamu za Kiswahili nchini Tanzania. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Chuachua, R. (2016). Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu. Tasnifu ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Deme, M.K. (2009). Heroism and Supernatural in African Epic Towards a Critical Analysis. Katika *Journal of Black Studies*, Juz. 39, 3: 402- 419.

Ilomo, I.F. (2013) *African Religion: A Basis for Interfaith Dialogue Today*. Dar es Salaam Tanzania: Dar es Salaam University Press.

Johnson, J.W. (1992). *The Epic of Son-Jara: A West African Tradition, Notes Translation and New Introduction,* Bloomington: Indiana University Press.

Kagame, A. (1956). *La Philosophie Bantu-Rwandaise de L'Etre*. Bruxelles: Academie Rayoledes Sciences Coloniales.

Kezilahabi, E. (1985). African Philosophy and the Problem of Literary Interpretation. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Wisconsin Madison.

Lightfoot, D. (1980). Concepts of Destiny in Vergil's Aeneid. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Leicester.

Lyamuya, H.N. (2014). Ulinganishi wa Sababu za Kuanguka kwa Shujaa katika Utendi wa Kiswahili na Tendi Nyingine za Kiafrika. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mair, L. (1969). *Witchcraft*. London: World University Library.

Magesa, L. (1997). *African Religion the Moral Traditions of Abundant Life*. New York: Orbis Books.

Makumba, M.M. (2005). *Introduction to Philosophy*. Nairobi: Paulines Publications.

Mihanjo, A. (2004). *Falsafa ya Usanifu wa Hoja kutoka Wayunani hadi Watanzania (Waafrika).* Tanzania: SALVATORIANUM.

Mulokozi, M.M. (2002). *The African Epic Controversy: Historic, Philosophical and Aesthetic Perspectives on Epic Poetry and Performance*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Mbiti, S.S. (1969). *African Religion and Philosophy*. London: Heinemann University.

Mbiti, J. (1991). *Introduction to Africa Religion Second Edition*. Nairobi: East African Educational Publshers L.t.d

Mpalanzi, L. (2019). Ujitokezaji wa falsafa ya Kiafrika katika Riwaya za Kiethinografia za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Njogu, K. na Chimerah, R. (2008). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Autolitho Ltd.

Nkemnkia, M.N. (1999). *African Vitalogy: A Step Forward in African Thinking*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Okpewho, I. (1979). *The Epic in Africa Towards A Poetic of the Oral Performance*. New York: Columbia University Press.

Omokpo, V. na Ukwamedua, N.U. (2016). The Ontology of Destiny and Freedom among Igbo-Africans; A Discourse in Existential Metaphysics. Katika *IDEA*, Juz. Xxviii/2:273-286.

Ortega, A.S. (2016). *Fortune, Fate and Destiny in Shakespeare's Romeo and Juliet*. Universidad De Jaen: Departamento de Filologia Iglesa.

Pack, R.A. (1939). Chance and Tragic Error. Katika *The American Journal of Philosophy*, Juz. 60, 2: 350-356.

Ponera, A.S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.

Reehana, Sand, S. D., Ujjan, A. U., Turk, M. K., Detho, M.D., Nizamani, K. M., DuaUrooj, S.,

Panhwar, K. (2016). Role of Fate in Oedipus by Sophocles. Katika *International Researchers*, Juz. 5: 2:1-6.

Tempels, P. (1945). *La Philosophie Bantoue*. Paris: Presence Africaine.

Tempels, P. (1969). *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wiredu, K. (2006). *A Companion to African Philosophy*. Malden: Blackwell Publishing.